




# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



## JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na.16. Msimu wa Kilimo 2022/23

Tathmini ya Februari 21-28, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Machi 1-10, 2023

### MUHTASARI

- Hali ya ukavu iliyojitokeza kwenye maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka ilipunguza unyevunyevu katika udongo ambao umeathiri ukuaji wa mazao hususan mpunga na mahindi yaliyopandwa nje ya msimu.
- Kwa ujumla zao la mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hali ya kuridhisha.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanahimizwa kuzingatia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023


**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika kidogo wakati ile iliyoko kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilikuwa na mabadiliko kidogo. Hali hii iliendelea kuufanya ukanda mvua ITCZ, kuambaa katika baadhi ya maeneo nchini hususan maeneo yaliyoko kusini mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi lilikua la wastani hadi chini ya wastani na hivyo kutokuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi na kuelekea katika baadhi ya maeneo ya pwani ya nchi.

Kwa upande mwingine, upepo katika tabaka la chini ulivuma ukitokea magharibi na hivyo kuwa na mchango katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya

### TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023

**K**atika dikadi hii, baadhi ya maeneo ya nchi yalipata mvua chini ya milimita 10 isipokuwa katika maeneo ya kanda ya ziwa Victoria, magharibi na nyanda za juu kusini magharibi ambayo yalipata mvua zaidi ya milimita 10. Hata hivyo maeneo machache ya mkoa wa Mbeya yalipata mvua zaidi ya milimita 100 kama inavyoonekana katika kielelezo.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi Februari 21-28, 2023

### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023

**M**vuza zilizonyesha katika dikadi hii hususan katika maeneo yanayopata mvua za msimu zimeongeza unyevunyevu katika udongo ambao umesaidia ukuaji wa mazao.

Kwa ujumla mahindi katika maeneo yanayopata mvua za msimu yapo katika hali ya kuridhisha. Katika mkoa wa Kigoma na Tabora mahindi yapo katika hatua ya kukomaa.

Hali ya ukavu iliyojitokeza kwenye maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka ilipunguza unyevunyevu katika udongo ambao umeathiri ukuaji wa mazao hususan mpunga na mahindi yaliyopandwa nje ya msimu.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya ukuaji katika maeneo

ya mikoa ya Tabora, Mbeya, Morogoro, na Rukwa, ambapo wakulima wameendelea na palizi.

Kwa upande mwingine katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan Kagera, Shinyanga na Simiyu wakulima wanamalizia shughuli za uvunaji wa mahindi. Zao la viazi mviringo lipo katika katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori ulikuwa wa kawaida katika maeneo mengi nchini.

### HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023

**K**wa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde vimeendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea hususan katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2023

**K**atika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia ikiimarika kidogo. Hali ambayo inatarajiwa kuendelea kuchochea uwepo wa ukanda mvua (ITCZ) katika baadhi ya maeneo nchini hususan kusini mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani katika eneo kubwa na hivyo kutokua na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi kuelekea katika maeneo ya pwani ya nchi.

Katika tabaka la chini la anga, upepo unatarajiwa kuendelea kuvuma kutokea magharibi hususan katika nusu ya pili ya dekadi, hali inayotarajiwa kuendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka kwenye misitu ya Congo kuelekea nchini hususan maeneo ya magharibi mwa nchi.

### HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2023

**M**aeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua na ngurumo za radi.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mikoa wa Morogoro) zinatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

### HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2023

**M**aeneo ya pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi.

vua zinazotarajiwa hususan katika maeneo yanayopata mvua za msimu zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Wakulima katika maeneo hayo wanashauriwa kuendelea na shughuli za palizi, uwekaji mbolea, kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, kwa ajili ya maziwa makuu na baharini ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

### HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2023

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.